HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO.

MUHTASARI WA KIKAO **CHA TIMU YA WATAALAM** KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 20/10/2021.

WAJUMBE WALIODHURIA:

1.	Bw. Chiriku H. Chilumba	- Mkurugenzi Mtendaji (W)	- Mwenyekiti
2.	Elionora Lyimo	- Kaimu Afisa Utumishi na Utawala (W)	- Katibu
3.	Bw. Ambokile Paul	- Afisa Mifugo na Uvuvi (W)	- Mjumbe
4.	Bw. Peres Kamugisha	- Afisa Maendeleo ya Jamii (W)	- Mjumbe
5.	Bw. Amos Kanige	- Kaimu Afisa Mipango (W)	- Mjumbe
6.	Bi. Roza Nabahani	- Afisa Elimu Sekondari (W)	- Mjumbe
7.	Bw. Hyazint Mbiro	- PSSNC TASAF	- Mjumbe
8.	Bw. Sambalu Simon	- Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W)	- Mjumbe
9.	Bw. Estery Mwinuka	- Kaimu Afisa Uchaguzi	- Mjumbe
10.	Bw. Adrew Tarimo	- Kaimu Afisa Kilimo na Umwagiliaji (W)	- Mjumbe
11.	Dr. Lucia Kafumu	- Mganga Mkuu (W)	- Mjumbe
12.	Bw. Bakari Nihuka	- Kaimu Mweka Hazina (W)	- Mjumbe
13.	Bw. Samson Manjale	- Kaimu Afisa Manunuzi (W)	- Mjumbe
14.	Bw.Protas Komba	- Afisa Elimu Msingi (W)	- Mjumbe
15.	Bw. Edwin Swai	- Afisa TEHAMA	- Mjumbe
16.	Bw. Geofrey S. Kalikawe	- Mtendaji wa Mamlaka M/M Namtumbo	- Mjumbe
17.	Bw. John Mwingira	- Mkaguzi wa Ndani (W)	- Mjumbe
18.	Bw. Venance Hanje	- Kaimu Afisa Sheria (W)	- Mjumbe
19.	Bw. Revocatus Kavishe	- Afisa Biashara (W)	- Mjumbe
20.	Bw. Yerermias Ngerangera	- Afisa Habari	- Mjumbe
21.	Bw. Kinonono HS	- Kaimu Mhandisi Ujenzi (W)	- Mjumbe

WATAALAM WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA:-

Hakuna

SEKRETARIETI:

1.	Bw. Solomon Hyera	- Mwandishi wa Vikao	- CC
2.	Bi. Benadetha Ndunguru	- Mwandishi wa Vikao	- CC

KUMBU NA - NMT/CMT/03/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO.

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao, kabla ya kufungua kikao Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao na kuwaomba kujadili juu ya utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa madarasa kupitia fedha za UVIKO-19 katika shule za sekondari ,shule shikizi za msingi pamoja na nyumba ya Mganga, kisha alifungua kikao saa 04:15 asubuhi.

Scanned with CamScanner

KUMBU NA - NMT/CMT/03/2021/2022: KUSOMA NA KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 20/10/2021.

Wajumbe walisomewa agenda za kikao cha tarehe 20/10/2021 na baada ya kusomwa agenda, Wajumbe waliridhia agenda zifuatazo kujadiliwa katika kikao hicho.

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia agenda
3. Mpango kazi wa wilaya kutekeleza miradi ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano ya UVIKO – 19
4. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti.
5. Kufunga kikao

DONDOO NMT/KAZI/05/2021/2022: MPANGO KAZI WA WILAYA KUTEKELEZA MIRADI YA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO YA UVIKO - 19

Taarifa iliwasilishwa akieleza juu ya mapokezi ya fedha Tsh 1,720,000,000.00 kwaajili ya utekelezaji na ujenzi wa madarasa katika shule za sekondari na Msingi Taarifa iliendelea kueleza kuwa fedha zilizotolewa ni kwaajili ya ujenzi na sio kilipana posho Taarifa ilieeleza kuwa madarasa yatakayojengwa ni 80 shule ya sekondari madarasa 6 shule shikizi pamoja na nyumba ya Mganga 3 in 1.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walichangia kutoa maagizo na maelekezo kama ifuatavyo Wajumbe waliagiza kitengo cha manunuzi na idara ya fedha kuhakikisha inafanyakazi kwa weledi na kama kuna makosa yaliwahi kujitokeza katika miradi iliyopita yasirudiwe tena

- Katika kutekeleza miradi hiyo wajumbe waliagiza kuwa wananchi hawaruhusiwi kuchangishwa fedha kwani fedha zilizotolewa zinatosha kukamilisha majengo yote pia alieleza majengo yote yajengwe kwa tofali za saruji (blocks),na ikikamilika iwekwe ,gypsum (sio bati) pia majengo yote yahakikishwe yanawekwa marumaru (tiles)
- kulingana na muda kuwa mchache wajumbe walikubaliana kamati zote za ujenzi zitaundwa mara baada ya baraza la madiwani litakalo fanyika tarehe 29/10/2021
- Kutokana na uharaka na umuhimu wa miradi hiyo Wajumbe walikubaliana kuwa matangazo ya kazi katika ujenzi wa miundombinu kuanza kutolewa kuanzia tarehe 28/10/2021 ili wenye sifa wapatikane mapema na taratibu nyingine ziweze kuendelea.
- Wajumbe walikubaliana kuwa miradi yote ianze kutekelezwa kuanzia tarehe 09/11/2021 na kumalizika ifikapo tarehe 15/12/2021
- Wajumbe walisisitiza kuhakikisha katika uteuzi wa mafundi wachaguliwe mafundi ambao wanauwezo ilikuwa na miradi bora na sio bora mradi
- Wajumbe walisisitiza kuwa fedha ni kwaajili ya ujenzi wa majengo mapya hivyo jengo lianzie msingi na sio kuanza na msingi wa zamani.
- Wajumbe waliongeza kuwa katika uundwaji wa kamati wajumbe wa kamati husika wahakikishwe wanapewa na majukumu kulingana na kamati aliyochaguliwa ili aweze kutambua na kutekeleza majukumu yake ipasavyo.
- Wajumbe walikubaliana kuwa idara zote zenye miradi zihakikishwe zinapanga ratiba ya kutembelea miradi hiyo kuanzia mwanzo wa mradi mpaka ukamilishwaji wake

Scanned with CamScanner

- Wajumbe walikubaliana kuwa kwa yeyote anayohusika endapo atashindwa kutekeleza majukumu yake au kutumia fedha za serikali kinyume na malengo yaliyopangwa atachukuliwa hatua za kisheria
- Wajumbe walikubaliana kila mkuu wa idara na kitengo akabidhiwe jengo moja kwa ajili ya ufuatiliaji wa karibu pia kutolea taarifa maendeleo ya mradi kila siku (kila hatua ya mradi unapofikia)

KUMBU NA - NMT/CMT/03/2021/2022: KUFUNGA KIKAO.

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao, kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti alihimiza yote yaliyoagizwa katika kikao hicho kufanyiwa kazi kwa wakati,kisha Mwenyekiti alifunga kikao saa 08:45 Mchana.

UMETHIBITISHWA,

.....
SAINI YA MWENYEKITI

.....
SAINI YA KATIBU

TAREHE ...../11/2021.

Scanned with CamScanner

HALMASHAURI YA WILAYA NAMTUMBO

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Simu: Na. 025 – 2675008
Fax: Na. 025 - 2675008
Email:-ded@namtumbodc.go.tz

P.O.BOX 55,
NAMTUMBO,
RUVUMA.

CIRCULAR RESOLUTION

KUTOKA\: Kitengo cha Manunuzi

KWENDA: Bodi ya Zabuni

TAREHE: 2/2/2022

YAH: KUOMBA IDHINI YA KUTUMIA NJIA YA FORCE ACCOUNT KATIKA UJENZI WA NYUMBA YA WATUMISHI LIKUSANGUSE

Kitengo cha Manunuzi kilipokea dokezo toka kwa Mkurugenzi kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba ya watumishi (3-in one) Likusanguse.

Awali kazi hii ilitangazwa kwenye Mfumo wa TANePS na Mkandarasi alipatikana Miracle squard kwa gharama ya Tshs. 127,334,500.00. Lakini kwa bahati mbaya Mkandarasi aliyekuwa amependekezwa ameshindwa kuendelea na kazi hii.Hivyo naleta kwenye kuombva Idhini ya kusitisha kuendelea na mchakato kwa kuingia mkataba na Mkandarasi.
Hata hivyo naleta kwenu kuomba idhini ya kutumia njia ya Force Account kama ilivyoelekezwa kwenye Mwongozo, endapo tutashindwa kupata Mkandarasi, tujenge kwa kutumia Force Account.
Kitengo cha Manunuzi kinaleta kwenu maombi ya kusitisha kuendelea na mchakato wa kuingia mkataba na Miracle Squard, pia naomba idhini ya kutumia wa njia ya force account ili tutekeleze mradi huo.

Kwa Mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013 pamoja na Marekebisho ya 2016 sehemu ya 58 Kifungu kidogo 1-4, maamuzi ya Bodi ya Zabuni yanaweza kufikiwa bila kukutana kwa njia ya "Circular Resolution" kwa kuzingatia hilo Kitengo kinaomba wajumbe wa Bodi ya Zabuni kuridhia maombi haya.

NA.	JINA LA MJUMBE	NAFASI	KUKUBALI	KUKATAA	SAHIHI
1	PERES KAMUGISHA	M/KITI	✓		

Scanned with CamScanner

2	SIMON SAMBALU	MJUMBE	✓		
3	ROZA NABAHANI	MJUMBE	✓		
4	PROTAS KOMBA	MJUMBE	✓		
5	AMOS KANIGE	MJUMBE	✓		
6	VENANCE HANJE	MWANASHERIA	✓		

.....

SAMSON MANJALE
KATIBU BODI YA ZABUNI
NAMTUMBO

Scanned with CamScanner